**Shirika la Kimataifa la Vyama vya Watoa huduma za Viwanda na Sanaa.**

**Chama cha Kisekta cha Muungano wa Kimataifa wa Vyama vya Ushirika (ICA)**

# AZIMIO LA DUNIA KUHUSU VYAMA VYA USHIRIKAVYYA WAFANYAKAZI

**Limepitishwa na Bunge kuu la ICA huko Cartagena, Columbia, tarehe 23 Septemba, 2005.**

*Azimio hili litafasiliwa kwa lugha mbalimbali za dunia, kwa kuzingatia utamaduni mbalimbali, taratibu za lugha na misemo ya vyama iliyotumika kwa misingi ya lugha chanzi, Kiingereza au Kihispania au zote.*

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. Wakati wote binadamu hutafuta njia bora za kupanga kazi na hutarajia kupata mafanikio na uhusiano na wa haki kazini.
2. Kwa sasa, watu hufanya shughuli zao za kazi kwa namna tatu.
   (a) Kwa kujitegemea kama wafanyakazi wa kujiajiri, wakitambuliwa kwa kuzingatia uwezo wao na kujiendesha kwa taratibu zao.
   (b) Kama wafanyakazi wa kulipwa mshahara, wakati wote wakiwa chini ya mamlaka ya mwajiri ambaye hutoa malipo ambayo hutolewa tu baada ya makubaliano na mtu binafsi au kikundi cha watu.
   (c) Katika aina ya tatu ambayo inaitwa umilikaji wa wafanyakazi ambapo kazi na usimamizi vinafanywa kwa pamoja, bila kuwa na mipaka maalumu ya kazi ya mtu mmoja wala kuwa chini ya Kanuni za kawaida za kazi kama za mkataba wa kulipwa mshahara.

3. Miongoni mwa aina za umilikaji wa wafanyakazi, umilikaji mmojawapo unaopangwa kupitia vyama vya Ushirika vya wafanyakazi umefikia hatua kubwa ya maendeleo na umuhimu wake kwa sasa umeongezeka duniani. Unaundwa kwa misingi ya kanuni za vyama vya ulimwengu, maadili na mbinu za kazi zilizomo

Hakimiliki(C)CICOPA 2004

kwenye Tamko la Manchester la 1995 kuhusu Utambuzi wa Vyama Vya Ushirika vya Wafanyakazi, lililokubaliwa katika mfumo wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika Duniani (ICA) na kuunganishwa kwenye pendekezo la ILO la 193/ 2002 kuhusu Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika vya Wafanyakazi.

4. Vyama vya Ushirika vya wafanyakazi vinatakiwa kuongozwa na Tamko linalohusu utambulisho wa Vyama vya Ushirika. Zaidi ya hayo, imekuwa muhimu kutoa ufafanuzi kwenye kiwango cha dunia na baadhi ya sifa zake bainifu za msingi na kanuni za ndani za kazi ambazo ni za kipekee katika vyama vya aina hii, vyenye madhumuni na malengo mahsusi ambayo yanatofautiana na ya Vyama vya Ushirika vya aina zingine. Ufafanuzi huu utaimarisha mshikamano na utambuzi wa dunia kuhusu umilikaji wa vyama vya ushirika vya wafanyakazi na utachochea maendeleo yake na kusababisha kutambuliwa kwenye kiwango cha dunia hususani kazi yake ya kijamii na kiuchumi katika kuibua kazi zenye hadhi na zilizo endelevu na wakati huohuo kuzuia migogoro au ugomvi.

5. Azimio la Dunia pia linahitajika ili kutilia mkazo umuhimu wa umilikaji wa Vyama vya Ushirika vya wafanyakazi, kuhamasisha Vyama vya Ushirika vya wafanyakazi na uhusiano wake na Vyama vya Wafanyakazi vya aina zingine pamoja na serikali, mashirika ya Kimataifa, ulimwengu wa ujasiriamali na vyama vya wafanyakazi. Hii ni muhimu kwa kuhakikisha maendeleo na ukuzaji wa vyama vya ushirika vya wafanyakazi pamoja na utambuzi kamili wa wajibu wao, kama watendaji katika kutafuta masuluhisho ya matatizo ya ukosefu wa ajira na kutoshirikishwa kwa jamii na kama watetezi wa chama kilichoendelea sana katika masuala ya kutetea haki, utu, uhusiano wa wafanyakazi, uzalishaji na usambazaji wa mali na umilikaji wa uchumi kwa kuzingatia demokrasia.

6. Ingawa CICOPA pia inajumuisha vyama binafsi vya wasanii na vya aina zingine za usimamizi wa vyama vya ushirika ambao unatokana na dhana kuu za kazi na uzalishaji, Azimio la sasa linalenga hasa kwenye vyama vya ushirika vya wafanyakazi. Hii haizuii uwezekano wa kutumiwa na watumiaji wengine, vyama ambavyo pia hutoa uanachama na umilikaji kwa wafanyakazi wake kama sehemu

inayowatofautisha na wanachama wengine kiasi kwamba maslahi yao yanawakilishwa inavyotakiwa. Pamoja na aina zote za usimamizi zinazoonyesha utambuzi maalumu wa kazi ya binadamu na wale wanaoifanya, kama vyama vya wafanyakazi vyenye mipaka ambavyo hutumia manufaa ya ushirika kwa ajili ya wafanyakazi wake na miradi yote ya kijamii kwa ujumla ambayo huleta uhusiano wa kipekee kwa wafanyakazi licha ya kuwapatia huduma za ustawi.

***Kwa misingi ya mambo yaliyotajwa hapo juu, CICOPA inapitisha bila kupingwa Azimio lifuatalo la Dunia kuhusu Vyama vya Ushirika wa Wafanyakazi.***

## I. SIFA ZA MSINGI

Kwa kuzingatia ufafanuzi, maadili na kanuni zilizomo kwenye Tamko kuhusu Utambulisho wa Vyama vya Ushirika (la mwaka 1995) na kuunganishwa kwenye mapendekezo ya ILO ya 193/2002 kuhusu Uendeshaji wa vyama vya Ushirika, Vyama vya Ushirika vya Wafanyakazi vina sifa za Msingi zifuatazo:

1. Vina lengo la kubuni na kuendeleza kazi endelevu na kuzalisha mali ili kuongeza ubora wa maisha ya wafanyakazi wanachama, kuboresha kazi za binadamu, kuruhusu usimamizi wa kidemokrasia wa kujisimamia na kukuza maendeleo ya ndani na ya jamii.

2. Uanachama huru na wa kujitolea katika kuchangia kwa kutumia kazi zao binafsi na rasilimali zao za kiuchumi kutategemea upatikanaji wa ajira.

3. Kama kawaida, kazi hufanywa na wanachama. Hii inamaanisha kuwa wengi wa wafanyakazi katika ushirika wa wafanyakazi fulani ni wanachama na kinyume chake.

---

[1] *"Ushirika ni Chama huru cha watu walioungana kwa hiari kufanikisha mahitaji yao ya kawaida ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni na kina matarajio kupitia chombo wanachomiliki pamoja na kinachodhibitiwa kisheria" (ILO)*

4. Uhusiano wa wanachama na ushirika wao unachukuliwa kuwa ni tofauti na uhusiano katika kazi za kulipwa mshahara au kazi ya kujiajiri.

5. Sheria zao za ndani ya chama kwa kawaida zinafafanuliwa kwa utaratibu ambao unakubaliwa kidemokrasia na kukubaliwa na wanafanyakazi wanachama.

6. Vina wanachama walio huru na wanaojitegemea kwa serikali na washirika wao katika uhusiano wa kazi na utawala na katika matumizi na usimamizi wa nyenzo za uzalishajimali.

## II. KANUNI ZA UTENDAJI WA NDANI

Katika utendaji wake wa ndani vyama vya ushirika vya wafanyakazi ni lazima vizingatie kanuni zifuatazo:

1. Kulipa mshahara kwa wanachama wake kwa usawa, kwa kuzingatia aina ya kazi, majukumu, ugumu wa kazi na nafasi za vyeo vyao, uzalishaji wao na uwezo wa kiuchumi wa mradi na kujaribu kupunguza tofauti kati ya mshahara wa juu na wa chini.

2. Kuchangia ongezeko la mtaji na kuwezesha ongezeko linalofaa la vyanzo vya fedha visivyo bayana na fedha.

3. Kutoa nyenzo halisi na za kiufundi mahali pa kazi zitakazofanikisha kufikia utendaji wa kiufanisi na hali nzuri ya chama.

4. Kulinda wafanyakazi wanachama kwa kuwaingiza kwenye mifumo inayofaa ya ustawi, usalama wa jamii na Afya kazini na kuzingatia viwango vya ulinzi vilivyopo kwenye maeneo ya wazazi, utunzaji wa watoto na watoto wadogo kazini.

5. Kutumia demokrasia katika kufanya uamuzi wa mambo ya ushirika na katika hatua zote za mchakato wa usimamizi.

6. Kuhakikisha wanachama wanapata elimu ya kudumu na mafunzo kwa ajili ya kuwaongezea uwezo wanachama. Kuhakikisha wanapata taarifa ili kuhakikisha kuwa wanaongeza maarifa ya kitaaluma, wanakuwa mfano bora wa wanachama wa ushirika wanaochochea uvumbuzi na usimamizi mzuri.

7. Kuchangia katika kuboresha hali ya maisha ya familia asilia na maendeleo endelevu ya jamii.

8. Kupigania kuwa watumishi waliodhamiria kubadilisha hali za wafanyakazi walioajiriwa na kuhakikisha wanaondokana na kuachana na kuwa wasuluhishi wa kazi za mikataba.

## III. UHUSIANO KATIKA VUGUVUGU LA USHIRIKA

Mwaliko wa nguvu unatolewa kwa ajili ya vuguvugu la ushirika kwa jumla ili:

1. Kutangaza vyama vya ushirika vya wafanyakazi ndani ya chama cha Ushirika Duniani na kuchangia kwa ufanisi ubunifu wa shughuli za aina hii.

2. Kuanzisha Muungano wa kimkakati ambao unachochea maendeleo ya ushirika wa wafanyakazi na kuifanya miradi yake, ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kutenga fedha na utangazaji wa huduma wanazozitoa na wa bidhaa wanazozalisha.

3. Kuanzisha utaratibu wa kutafuta mtaji katika ushirika wa wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kutoa michango ya dhima katika shirika kutoka kwenye vyama vya aina zingine za Ushirika, kwa kutumia malipo mbadala ya kiuchumi na ushiriki halali katika usimamizi bila kuhatarisha uhuru wao.

4. Kuendeleza wakala wa vyama vya ushirika vya wafanyakazi vya ngazi ya chini, kanda, kitaifa na kimataifa. Kukuza ushirikiano miongoni mwao na kusaidia uanzishaji wa vyama au vikundi vingine vya ujasiriamali, muungano wa vikundi na makubaliano ya kawaida ya kijamii na kiuchumi miongoni mwa vyama vya

ushirika ili kutoa kwa ufanisi huduma za kiujasiriamali, kuimarisha vuguvugu la ushirika na kupania kuwa na jamii ya mfano yenye sifa za ushirikiano na mshikamano.[2]

5. Kuendeleza juhudi ili kuhakikisha kuwa serikali katika ngazi zake inatoa na kuboresha nyenzo za maendeleo ya ushirika wa aina hii ikiwa ni pamoja na utungaji wa sheria zinazohusika na zinazofaa. Hii pia inamaanisha kupeleka maombi ya haki mbele ya wabunge ili sheria ipitishwe.

6. Kuendeleza kwa haraka kadiri iwezekanavyo muungano wa wafanyakazi wa ushirika, walioajiriwa wafanyakazi wanachama.

## (IV) UHUSIANO NA SERIKALI NA ASASI ZA KIKANDA NA ZA KISERIKALI

1. Serikali inapaswa kuelewa umuhimu wa kukuza na kuendeleza vyama vya ushirika vya wafanyakazi kama vyanzo vya kiufanisi vya ubunifu wa ajira na vinaunganisha vikundi vya watu wasio na ajira katika kazi.

   Kwa sababu hii, serikali zisibague vyama vya ushirika vya wafanyakazi na viingize shughuli za ukuzaji na uendeshaji wa vyama vya aina hii kwenye sera na programu zake ili kutatua baadhi ya matatizo makubwa ambayo dunia inakaribiana nayo, ambayo ni kama matokeo ya utandawazi na maendeleo kwa mfano, ukosefu wa ajira na vitendo vya ubaguzi.

2. Ili kuwa na umilikaji wa ushirika wa wafanyakazi chombo halisi, serikali lazima iandae mipango ya kitaifa na kikanda ya udhibiti, inayotambua na kuzingatia hali halisi ya vyama vya ushirika vya aina hii, inayoruhusu vyama kuzalisha bidhaa na kutoa huduma wakati hali inaporuhusu na kuendeleza ubunifu na uwezo wao wote wa kiujasiriamali kwa maslahi ya wafanyakazi wanachama na jamii kwa ujumla.

---

2 *"Uchukuaji wa hatua muhimu uhimizwe ili kuwezesha vyama vya ushirika, kama miradi na vyama vilivyohimizwa na mshikamano, kuitikia kuhusu mahitaji ya wanachama wake na mahitaji ya jamii ikiwa ni pamoja na yale ya vikundi ili kufikia ushirikishwaji katika jamii"*(Pendekezo la ILO la 193/2002 kif. 5)

3. Hasa, serikali inapaswa:

   - Katika sheria zake kutambua kuwa umiliki wa ushirika wa wafanyakazi na kazi zao unategemea uhusiano wa wafanyakazi na kazi zao ambazo zinatofautiana zikiwemo kazi za kulipwa mshahara na za kujiajiri au kazi za kujitegemea, na kukubali kwamba vyama vya ushirika vya wafanyakazi hutumia taratibu na mifumo inayofanana.
   - Kuhakikisha kuwa matumizi ya sheria za kawaida kwa wafanyakazi wasio wanachama wa vyama vya ushirika ambazo wao huanzishwa kwa ajili ya kazi za kulipwa mshahara kwa mkataba.
   - Kutumia kwa vyama vya ushirika vya wafanyakazi dhana ya ILO ya kazi zenye hadhi na masharti yanayoeleweka yenye ukweli na yanayoongoza ulinzi wa jamii katika vipengele vya Afya, pensheni, bima ya ukosefu wa ajira, afya kazini na usalama wa kazi kwa kuzingatia uhusiano wao kazini.
   - Kufafanua kanuni mahsusi za kisheria zinazoongoza mfumo wa fedha na chombo kinachojisimamia cha vyama vya ushirika vya wafanyakazi ambacho kinaweza kuleta na kuendeleza maendeleo yake.

4. Serikali inapaswa kuhakikisha upatikanaji wa hali nzuri ya fedha kwa ajili ya miradi ya ujasiriliamali iliyozinduliwa na vyama vya ushirika vya wafanyakazi kwa kuanzisha mifuko maalumu ya fedha za umma au udhamini wa mikopo au mikataba kwa ajili ya upatikanaji wa fedha na kukuza muungano wa kiuchumi na vuguvugu la ushirika.

5. Serikali na mashirika ya kikanda na ya serikali ni lazima yaendeleze miradi inayolenga kwenye kubadilishana uzoevu mzuri kwa taarifa, kuhusu maendeleo ya mifumo ya ujasiriamali na misaada wa kiasasi kwa ajili ya vyama vya ushirika vya wafanyakazi katika uwanda wa uhusiano wa Kimataifa na kikanda, kwa ajili ya upatikanaji wa ajira, juhudi endelevu za kiujasiriamali, usawa wa jinsia na kupigana vita dhidi ya umaskini na ubaguzi.

6. Umilikaji wa vyama vya ushirika vya wafanyakazi unapaswa kuendelezwa kama njia na mfano wa ujasiriamali katika mchakato wa mabadiliko ya kibiashara na uundaji unaanzia hapo, ubinafsishaji, ubadilishaji wa miradi iliyo hatarini na uendelezaji wa miradi isiyo na warithi kama katika makubaliano ya huduma na ugavi kwa umma ambamo serikali inapaswa kutoa ufafanuzi wa masharti ambayo yanachochea maendeleo ya eneo hilo kutokana na miradi ya ushirika wa wafanyakazi.

7. Katika muktadha wa uhusiano na serikali, ni muhimu kuonyesha Mwongozo wa Pendekezo la ILO la 193 linalohusu umuhimu wa kufanya juhudi katika uimarishaji wa eneo muhimu la uchumi ambalo linajumuisha vyama vya ushirika.[3] Ni eneo ambamo faida siyo motisha ya kwanza, lina sifa ya mshikamano, ushirikishwaji na demokrasia ya kiuchumi.

## V. UHUSIANO NA VYAMA VYA WAAJIRI

Vyama vya waajiri vinaweza kukuza maendeleo ya umilikaji wa vyama vya ushirika vya wafanyakazi katika mfumo wa kiujasiriamali ambao lengo lake kuu ni utafutaji wa ajira endelevu na zenye hadhi na ongezeko la thamani inayotokana na ubunifu, na kama mkakati sahihi wa kufufua miradi iliyo hatarini au katika mchakato wa kulipa madeni wakati wakiheshimu uhuru, wakiruhusu maendeleo yao ya ujasiliamali na bila kutumia vibaya utaratibu huu wa kiuhusiano katika kazi katika kukiuka haki za kazi za wafanyakazi.

[3]. *"Jamii yenye usawa hulazimisha uwepo wa sekta ya umma na sekta binafsi, pamoja na ushirika imara wenye pande mbili, na sekta nyingine ya kijamii isiyo ya serikali".* (ILO R. 193, art. 6)

## (IV) UHUSIANO NA VYAMA VYA WAFANYAKAZI

Vuguvugu la ushirika lazima liendeleze mjadala wa kudumu na vyama vya wafanyakazi ambavyo ni wawakilishi wa wafanyakazi ili kuhakikisha kwamba wanaelewa hali na umuhimu wa umilikaji wa vyama vya ushirika vya wafanyakazi kama mfumo wa kipekee wa uhusiano wa wafanyakazi na umilikaji[4] kwa kupambana na migogoro halisi ya kazi za kulipwa mshahara na kwamba vinasaidia mfumo huo kwa kuzingatia umuhimu wake na matarajio unayoyatoa kwa jamii.

***Azimio hili linaendana na Pendekezo la 193 la ILO lililopitishwa na Serikali, vyama vya waajiri na wafanyakazi duniani kote[5]. Kwa hiyo, tunaamini kuwa Azimio hili linazingatiwa kwa makini ili kuchangia ufumbuzi wa tatizo hili sugu la dunia la ukosefu wa ajira ambalo linaathiri utu na kuhatarisha amani ya dunia na haki za binadamu.***

---

[4] *Kuhusu hili, Pendekezo la ILO la 193/202 linaeleza kuwa "vyama vya 'wafanyakazi' vihimizwe (.....) kuendeleza zoezi la kutetea haki za wafanyakazi wanachama wa vyama vya wafanyakazi"* (art. 16 g)

[5] *Pendekezo linaeleza kuwa "Uendelezaji wa vyama vya ushirika (....) uchukuliwe kama nguzo mojawapo ya maendeleo ya jamii na uchumi wa Kitaifa na Kimataifa"* (art. 7 (1) ).